MCHANGANUO WA BAJETI YA VIJANA, 2021

FURSA YA AJIRA KWA VIJANA TANZANIA: HALI YA BAJETI YA TAIFA 2021-2022

MCHANGANUO WA BAJETI YA VIJANA, 2021: FURSA YA AJIRA KWA VIJANA, TANZANIA: HALI YA BAJETI YA TAIFA,2021-2022:

Hali ya ukosefu wa ajira kwa Vijana

Ifikapo mwaka 2030, takriban 1/3 ya nguvu kazi ya vijana duniani, watatoka Afrika. Hata hivyo, mwaka 2020 ulishuhudia wanawake waliokosa ajira wakiwa ni wengi zaidi (asilimia 7.5) kuliko wanaume (asilimia 6.3) hali ambayo ilijidhihirisha pia kwenye nchi kadhaa duniani. Kwa mfano Afrika Magharibi ilishuhudia ukosefu wa ajira kwa wanawake ukiwa kwenye kiwango cha asilimia 6.6, ukifananisha na asilimia[1]5.6 kwa wanaume.

[1] ILO Report on employment in Africa (Re-Africa).

Kulingana na sensa ya Tanzania ya mwaka 2012, asilimia 77 ya Watanzania wapo chini ya miaka 35 na asilimia 19 wapo kati ya miaka 15-24. Kiwango cha ukosefu wa ajira kati ya vijana wenye umri wa miaka 15–24 ni asilimia 13.4. Ukosefu wa ajira umekuwa pia mkubwa kwa vijana wa kike, ikiwa ni asilimia 14.3 tofauti na wale wa kiume wenye asilimia 12.3.[2] Hata hivyo, kwenye ripoti ya Takwimu za Taifa (NBS) ijulikanayo kama **"2019 Tanzania Kitarakimu"** ya Juni 2020 inaonesha kuwa hali ya ukosefu wa ajira, ilishuka kutoka asilimia 10.1 mwaka 2015 mpaka asilimia 9.6 mwaka 2019.[3]

Takwimu zinaeleza zaidi kwamba, ukosefu wa ajira kwa vijana wa kike ni asilimia 12.3 ukilinganisha na vijana wanaume ambao ni asilimia 8.2. Vijana wenye umri wa miaka 15-24 wana nafasi ndogo kwenye ajira, (asilimia 13.7) ukifananisha na makundi mengine, na hiyo inafuatiwa na wazee miaka 65 na zaidi, wakiwa na asilimia 10.8. Takwimu zinaendela kuonesha zaidi kwamba, vijana wenye elimu ya Sekondari, wana nafasi ndogo zaidi ya ajira, ikiwa ni asilimia 13.8 ikifuatiwa na vijana waliomaliza shule ya msingi kwa asilimia 10. Wakati huohuo, wale wenye elimu ya vyuo (sio vyuo vikuu) wana nafasi nzuri za ajira, na ni asilimia 4.9 tu wanakosa kazi. Kwenye viwango vya elimu, ukiwaondoa wale wenye elimu ya vyuo na ambao sio wa Vyuo Vikuu, ukosefu wa ajira kwa wanawake ni mkubwa kuliko wanaume.

[2] The 2012 Census Report

[3] https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/references/Tanzania_in_Figures_2019.pdf

Sera

Vijana wengi wakiwa kwenye umri wa miaka 20, ndio huanza ajira. Hata hivyo uamuzi wao wa kufanya kazi hasa kwa wale wa kike, una changamoto zake, kutokana na ukweli kwamba bado ni tegemezi. Changamoto hizo zinakuwa mbaya zaidi kwa nchi zile ambazo sheria na tamaduni zake haziruhusu wanawake kufanya kazi au kujitegemea. Hata kwa wale wanaoanza biashara zao binafsi ili wajitegemee, wana changamoto za mitaji kwa vile hawakubaliki kwenye taasisi za fedha kwa mikopo kwa kuwa bado ni wachanga na hawana rasilimali za kuweka kama dhamana (collateral) kama ilivyo kwa biashara kubwa na zilizoendelea. Kama ilivyoelezwa hapo juu, vijana wengi wasichana wanashindwa kupita kutafuta kazi au kwenda kwenye mahojiano, kutokana na kulazimika kuomba ruhusa kwa wanaowatunza au kama wameolewa, majukumu ya nyumbani yanawabana. Mbaya zaidi kijana wa kike kama ana mtoto au watoto, atawaacha na nani anapokuwa kazini? Hii ni changamoto kwa hawa wasichana. Na hata kama alibahatika kupata kibarua, anapopata mtoto inabidi aache kibarua hicho na kulea mtoto. Malengo ya maendeleo endelevu (lengo la 5 na 8) yanaeleza ushiriki sawa wa wanaume na wanawake katika shughuli za kiuchumi. Hii inajumuisha pia usawa katika upatikanaji wa huduma za mikopo, na umiliki wa ardhi na mali zingine zenye tija katika uzalishaji.

Mkataba wa Vijana Afrika na Programu ya Umoja wa Mataifa kwa Vijana umekiri kwamba ukosefu wa ajira kwa Vijana wa Kiume na Kike, ni changamoto ya kupewa kipaumbele.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana Tanzania ya mwaka 2007 inaeleza kwamba kwa miaka yote, vijana wa kike wamekuwa hawapati ajira kama wenzao wa kiume. Hii ni kutokana na vizingiti katika upatikanaji wa elimu ya awali. Pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikijitahidi kuongeza idadi ya usajili kwa shule za awali kwa watoto wa kiume na wa kike, kiwango cha wasichana wanaoendelea na masomo ya sekondari na vyuo vya elimu ya juu imekuwa ikipungua na kukuta wanaomaliza vyuo ni wachache sana.

Mwaka 2018 Serikali za Mitaa ziliweka sheria ya fedha ili kuwezesha makundi ya watu wenye kipato cha chini kupata mikopo kwa ajili ya kufanya shughuli zenye kipato ili kuondoa umasikini na kupunguza ukosefu wa ajira. Hata hivyo sheria ya kupewa asilimia 10 ya mkopo kwa makundi hayo katika ngazi ya Serikali za Mitaa inakosa msukumo wa kuhakikisha kwamba vijana wa kike wanapata asilimia 4 ya mkopo kama inavyotakiwa kisheria ili kuwawezesha vijana hao wa kike. Kwa hiyo kuna haja kubwa ya kufuatilia na kutathmini ili kuona kama hizo fedha wanazipata na jinsi wanavyozitumia na kufaidika nazo. Hii iwe katika ngazi ya TAMISEMI na kwa wote, wakiume na kike. Inaeleza katika sehemu ya 37A kwamba mikopo hiyo itolewe kwa vikundi vilivyosajiliwa tu. Zaidi ya hapo, sharia Na. 3 inasema kwamba, ili kupata mkopo vijana watano (5) wasajiliwe kwa pamoja. Hata hivyo watu wenye ulemavu wanaweza kupata mkopo, kuanzia mtu mmoja. Hiyo inaleta, mkanganyiko ambao unahitaji Halmashauri kuwaandikia barua watoaji mikopo ili wale wanaohitaji mikopo bila kuwa na vikundi yaani mtu mmoja mmoja au wawili waidhinishiwe mikopo kwa barua hiyo badala ya cheti cha usajili ambacho kinakuwa na watu watano.

Mwelekeo kuhusu Makadirio ya Fedha kwa Vijana (Fedha za Serikali za Mitaa (4+4+2)

Tafiti zinaonesha kuwa taasisi za fedha zinawasahau wanawake. Kwa mfano mwaka 2017 jumla ya wahitaji 2,202 walipata mikopo toka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Kati yao asilimia 71.3 walikuwa wanaume na asilimia 28.7 walikuwa wanawake, ni kama 1 kwa 4. Hata hivyo fedha hizo za uwezeshaji zimekuwa mkombozi kwa wanawake. Tunatambua kwamba TAMISEMI imekuwa ikifuatilia utoaji wa fedha hizo kwa Wanawake,Vijana na Watu wenye ulemavu (PWDs) kufuatana na kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, na Kanuni za Uendeshaji wa Mikopo kwa makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu ya mwaka 2019. Katika mchanganuo huo, pamoja na upatikanaji wa fursa kwa vijana katika mwaka wa fedha 2021-2022, tunachanganua matokeo ya utekelezaji wa Sheria ya Fedha Serikali za Mitaa na kuona ni vijana wangapi wa kike wananufaika na Mfuko huo kwa biashara zao ili kuwa na maisha bora na familia zao. Kabla ya Sheria hiyo, mwaka wa fedha 2017/18, Mfuko wa Vijana na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulipewa shilingi bilioni 61.6 ambayo ni asilimia 10 ambazo ni fedha za Halmashauri kwa makundi 18,233. Mwezi wa Februari, 2018 jumla ya shilingi bilioni 15.16 ziligawiwa kwa makundi 8,672 ya Wanawake na Vijana, ikiwa ni asilimia 25 za fedha zilizotolewa.

Katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya shilingi bilioni 64.5 ziligawiwa kwa halmashauri nchini kama mikopo kwa vikundi 18,244 vya wanawake vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya hizo, kiasi cha shilingi bilioni 25.8 zilitolewa kwa vikundi 8,223 vya wanawake, Shs. 25.8 bilioni kwa vikundi 6,966 vya vijana na shilingi 12.9 bilioni kwa vikundi 3,055 vya watu wenye ulemavu.

Mnamo Februari 2021, jumla ya shilingi bilioni 26.81, sawa na asilimia 41.61 ya lengo la shilingi bilioni 64.46 ziligawiwa kwa makundi 5,973 ya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. Ndani ya mwaka huohuo 2021, TAMISEMI imerekebisha kanuni za utekelezaji wa asilimia 10 za uwezeshaji kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kwa kupunguza idadi ya watu wa kujisajili kwa kundi kutoka 10 hadi watano (5), ambapo kwa wasiojiweza kundi linaanzia na mtu mmoja. Sehemu ya fedha hizo zinatumika kwa ufuatiliaji wa makundi, tathmini, mafunzo ya ujasiriamali, uongozi, usimamizi wa fedha na uandikaji ripoti.

Katika ripoti ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2018-2019, makadirio kuhusu ufanisi wa fedha za malipo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ilibaini kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa 115 hazikuchangia kwenye mfuko kiasi cha shilingi bilioni 9,930,902,514, na pia Mamlaka 111 hazikurejeshewa kiasi cha shilingi bilioni 13,794,359,981 zilizotolewa kama mkopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na Watu wenye ulemavu.[4] Wakati katika kipindi cha mwaka 2019-2020, Mamlaka za Serikali za Mitaa 82 hazikuchangia asilimia 10 ya mapato yao ya ndani kwenye mfuko iliofikia shilingi bilioni 5,720,140,159, wakati shilingi

[4] https://www.nao.go.tz/uploads/mamlaka_za_serikali_za_mitaa_kwa_mwaka_wa_fedha_2018-2019.pdf

bilioni 27,790,189,049 zilizotolewa kama mkopo kwa makundi hayo hazikurejeshwa. Hali hii inaonesha kwamba Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazichangii kufikia asilimia 10 kama inavyotakiwa, na urejeshaji wa mikopo toka makundi husika unahitaji ufuatiliaji wa makini.

Fursa ya Bajeti ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Maendeleo ya stadi za vijana na uwezeshaji vimepewa kipaumbele kwa ufanikishaji wa malengo ya maendeleo ya Miaka Mitano ya 2021/2026. Kwa mwaka 2021/2022 Bajeti ya shilingi bilioni 77.66 zimetengwa kwa kuwawezesha vijana kupitia programu ya maendeleo ya stadi. Stadi hizo zitawawezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri, ambapo shilingi bilioni 67.66 ni kwa ajili ya kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kukuza ajira na kipato. Bilioni tisa (9) kwa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Stadi kwa Taifa, na bilioni moja (1) mikopo kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana.

Serikali imetoa shilingi bilion 13.3 kama sehemu ya maendeleo ya stadi kwa wanafunzi 2,650 katika ngazi ya cheti na diploma katika sekta ya kilimo ili kuwaandaa vijana kwenye stadi za kilimo cha kisasa. Kwa mfano, kwenda kidigitali katika kilimo, na uanzishwaji vituo vya ukuzaji/uleaji, Uyole,Ilonga,Tumbi na Ukiluguru. Uwekezaji huu utakuza na kuleta mapinduzi kwenye kilimo. Hata hivyo, pamoja na uwekezaji mkubwa kwenye kilimo, kuna haja ya kufanya tafiti za mara kwa mara ili kupima mtazamo na ushiriki wa vijana kwenye sekta ya kilimo. Kilimo kinachangia asilimia 58 ya nguvukazi nchini wengi wao wakiwa ni wanawake. Lakini pia, pato la nchi limeongezeka toka shilingi bilioni 25.2

Kielelezo 1



mwaka 2015 mpaka bilioni 29.5 mwaka 2019 ambao ni ukuaji wa asilimia 17 unaotokana na sekta mbalimbali ikiwemo kilimo. Kwa mfano serikali inatoa shilingi bilioni 15 kwa NFRA kwa ajili ya kununua nafaka kutoka kwa wakulima na pia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza bilioni 50 kwa nia hiyohiyo. Huu ni wakati kwa vijana kujikita katika sekta ya kilimo. Kilimo hiki kiende kidijitali kupitia M-Kilimo na agri-Dashboard ambavyo ni kipenzi cha vijana.

VETA imejikita kwenye kuongeza thamani na ufanisi kwenye vyuo vyao vya ufundi nchi nzima kwa kuongeza usajili wa wanafunzi toka 357,850 mpaka 500,000 ambapo wanafunzi 1,000 ni wenye ulemavu na 2,400 wasio kwenye mfumo rasmi watasajiliwa na kurasimisha stadi za takriban wanafunzi 10,000 ambao wataongeza nguvu, kuanzisha na kukuza takriban mitaala 10, ikijikita kwenye matakwa ya soko la ajira na kuimarisha njia ya kukusanya taarifa za soko la ajira. Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, elimu bure shule za msingi, kuimarisha Vyuo vya VETA, kuendeleza stadi za vijana na ujenzi wa miundombinu ya elimu kwa shilingi bilioni 406.6.

Katika harakati zake za kutekeleza wajibu wa mafunzo, Sekta ya Madini imepania kuongeza usajili wa muda mrefu na mfupi kwa wanafunzi wake katika sekta mbalimbali za madini, na kutoa ushauri kwa wadau wa madini. Vilevile Sekta hiyo ya madini, itafanya utafiti ukilenga kuongeza thamani, kufanya usonara kwa kutengeneza vitu vya mapambo na kuendesha mafunzo yakilenga zaidi, vijana waliomaliza shule za msingi ili nao waweze kujitegemea.

Pamoja na vijana wengi kujikita kwenye michezo, sekta hii ndogo inachangia asilimia 0.3 ya Pato la Taifa kati ya mwaka 2013-2019. Kwa mwaka 2020-2021, serikali imetenga shilingi bilioni 54.74 nyingi zikienda kwenye ujenzi wa miundombinu. Hata hivyo, kuna haja ya serikali kutenga fedha kwa kuendeleza stadi kwenye michezo na ubunifu. Hii iende sambamba na urasimishaji wa sekta hiyo ili kutathmini ni kiasi gani inachangia kwenye Pato la Taifa .

Hitimisho na Mapendekezo

Kwa ujumla, upatikanaji wa taarifa ya fungu la fedha zilizopo hazibagui jinsia. Hii ni changamoto kwa jamii ili kufahamu ni kiasi gani wanawake wananufaika na fedha hizo. Kwa hivyo tunahimiza serikali kutilia maanani suala la jinsia kwenye ripoti zake za takwimu. Kipaumbele kitolewe kwenye makundi yanayojumuisha Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu.

Tunahimiza pia Serikali ichukue hatua ya dhati, kutengeneza sera, na sheria imara kwa kudumisha usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa vijana wa kike katika kutekeleza mikopo kwa vijana. Hii inaweza kwenda sambamba na mapitio ya taratibu na gharama ya kurasimisha biashara za vijana. Na hii itafanya biashara zao zitambulike rasmi na kuweza kupata mikopo.

Kabla ya kutunga sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2017/18, fedha zilizotolewa zilikuwa bilioni 61.6, ambapo miaka mitatu baadaye, mwaka wa fedha 2020/21, ilikuwa bilioni 64.5. Hii inamaanisha kwamba kulikuwa na ongezeko la bilioni 3.1 tu. Hili ni ongezeko finyu ukilinganisha na idadi kubwa ya wasio na ajira

vya watu watano (5), lakini kwa watu wenye ulemavu wanaruhusiwa kupewa mkopo kama mtu mmoja au wawili au zaidi.. Kwa hivyo kuna kila sababu kwa Halmashauri kuwa na sheria itakayoruhusu watu wenye ulemavu kusajiliwa kama mtu mmoja,wawili,watatu na kadhalika. Hata hivyo, sera zinazoruhusu uzalishaji kwa mikopo ziende sambamba na bima ya afya. Hii itakomaza miradi ya vijana, hata kuzalisha ajira kwa wengine.

Tunazishauri Serikali za Mitaa kutoa mikopo na vivutio kwenye miradi mikubwa ya uzalishaji kwa kubadilisha na kuongeza teknolojia na kuleta ubunifu ili ziweze pia kuajiri watu wengi na kuongeza ajira kwa wanaume na wanawake. Hii inawezekana kwa kuweka sera za kiutendaji zitakazowainua vijana kuhitimu mafunzo yatokanayo na mpango wa mkopo wa mfuko unaotokana na mchango wa asilimia 4 wa Halmashuri kwa Mfuko wa Vijana.

REFERENCES

1. https://www.imf.org/en/publications/weo
2. ILO Monitor 4rd Edition, https://www.ilo.org/global/topics/coronavirus/lang--en/index.htm 4Employment Trends for Youth 2020, available at: https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcomm/
3. ILO Report on employment in Africa (Re-Africa).
4. The 2012 Census Report
5. https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/references/Tanzania_in_Figures_2019.pdf
6. Dr. Tulole Bucheyeki, Southern Highlands Zonal Director, Tari-Uyole Agricultural Center, as reported by Mwananchi 30/04/2021
7. Women, Business and The Law Report 2019: A decade of Reform.
8. Sustainable Development Goals, 2000
9. The United Nations World program of action for Youth
10. The national Youth Development policy 2007
11. KANUNI ZA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU (MAREKEBISHO) ZA MWAKA 2021
12. The local government finance act, 2018
13. Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa Mwaka 2017 cha Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)
14. Minister' PO-RALG Budget Speech 2021/2022
15. https://www.tra.go.tz/images/headers/chapter_290-the_local_government_finance_act-01.pdf
16. Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2021-2022
17. National Budget Speech for 2021-2022

YOUTH
JOBS!

YOUTH JOBS

policy forum

P.O. Box 38486,
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2780200
Email: info@policyforum.or.tz
Website: www.policyforum.or.tz